**Barabara ndani ya Hifadhi zinavyochangia kuangamiza wanyamapori**

**Na Albano Midelo**



BARABARA kupita ndani ya hifadhi imekuwa ni changamoto katika hifadhi  za wanyamapori hapa nchini na hata katika nchi nyingine zenye hifadhi na mapori ya wanyamapori.

Hali hiyo inachangia kupunguza idadi ya wanyamapori ambao wamekuwa wanagongwa na magari ambayo yanapita katika hifadhi hizo.

Utafiti umebaini kuwa barabara inapopita ndani ya hifadhi husababisha athari nyingi zikiwemo za kupoteza mamilioni ya fedha kutokana na wanyama kufa,uchafuzi wa mazingira,ikolojia na kufanyika utalii wa bure.

Hifadhi ya Taifa ya Mikumi ni moja ya hifadhi ambayo  baadhi ya wanyama adimu wanatoweka kutokana na  kugongwa na magari

yanayopita katika barabara ya kutoka Dar es salaam kwenda mikoa ya nyanda za juu kusini inayopita ndani ya hifadhi hiyo.

Takwimu zinaonesha kuwa wastani wa mnyama mmoja anagongwa kila siku katika hifadhi hiyo na katika kipindi cha kuanzia mwaka 1991 hadi mwaka 2015 takriban miaka 25,wanyama wa aina mbalimbali zaidi ya 3,435 walikufa kwa kugongwa na magari katika hifadhi ya Taifa ya Mikumi.

Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Mikumi, Donat Mnyagatwa anasema takwimu zilizopo zinaonesha kuwa mwaka 1992 wanyama 72 waligongwa na kufa ambapo mwaka 2015 pekee wanyama 237 waligongwa na kufa.

Kwa mujibu wa Mnyagatwa takwimu za wanyama waliogongwa na kufa zinaonesha kuwa mwaka 2007 wanyama 43, mwaka 2008 wanyama 82,mwaka 2009 wanyama 45, mwaka 2010 wanyama 19, mwaka 2011 wanyama 125, mwaka 2012 wanyama 111, mwaka 2013 132 na mwaka 2014 wanyama 351.

Chrispine Mwinuka wa Idara ya Ikolojia katika Hifadhi ya Taifa ya Mikumi anasema ikolojia ya hifadhi hiyo inaendelea kuharibika kila mwaka kutokana na baadhi ya abiria kutupa takataka wanapokuwa wanasafiri kwenye mabasi lakini pia baadhi ya magari yanamwaga mafuta barabarani ndani ya hifadhi ambayo yanaweza kuleta madhara kwa wanyama.

Hifadhi ya Taifa ya Mikumi ni miongoni mwa hifadhi kubwa za Taifa ambazo ni maarufu ndani na nje ya nchi ikiwa umbali wa kilometa 288 kutoka jijini Dar es salaam na ukubwa wa kilometa za mraba 3230.

Barabara kuu ya Dar es salaam kwenda mikoa ya nyanda za juu kusini hadi nchi jirani za Malawi na Zambia inapita katikati ya hifadhi ya Taifa Mikumi na kusababisha kuwa moja ya hifadhi nchini ambazo zinafikika kwa urahisi.

Magari ambayo yanapita katikati ya hifadhi hii mara kwa mara yamekuwa yanagonga wanyama kama vile swalapala, pundamilia na wanyama wengine waliopo ndani ya hifadhi hii ambapo kipande wa kilometa 50 cha barabara kipo ndani ya hifadhi ya mikumi.

Licha ya sheria kuwataka madereva wanapoingia ndani ya hifadhi kuendesha magari yao kwa kuzingatia mwendo uliowekwa yaani kilometa 50 kwa saa wakiwa ndani ya hifadhi,lakini uchunguzi umebaini kuwa baadhi ya madereva hawazingatii sheria hiyo badala yake wamekuwa wanaendesha kwa mwendokasi na kusababisha kugonga wanyama ambao ni rasilimali ya Taifa.

Pia sheria katika hifadhi za Taifa haziruhusu abiria au mtu yeyote kutupa takataka ndani ya hifadhi ikiwa ni pamoja na kuwapatia wanyama vyakula,lakini katika hali halisi baadhi ya abiria wamekuwa vinara wa kuwatupia wanyama vyakula au kutupa takataka ndani ya hifadhi kinyume cha sheria.

Baadhi ya abiria wanaposafiri katika mabasi wakifika katika eneo la hifadhi ya Mikumi wamekuwa wanalalamika kuwa siku hizi katika hifadhi hiyo wanyama wamepungua kwa kuwa hawaonekani kama ilivyokuwa zamani.



Inawezekana kupungua kwa wanyama hao kwa namna moja au nyingine kumesababishwa na magari kuwagonga wanyama hao na kusababisha vifo au kuwajeruhi.

Uhai wa wanyamapori ni jambo ambalo linamhusu kila mtanzania hivyo Wizara ya Maliasili na Utalii na Idara ya Wanyamapori ni lazima kufanya kila wanachoweza kuhakikisha kuwa wanyama wanaendelea kulindwa kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho.

Baadhi ya wanyama ambao ni kivutio cha watalii katika hifadhi ya Taifa ya Mikumi ni chui, simba, mbwamwitu, twiga, nyati, tembo, kongoni, tandala mdogo, pofu, nguruwepori, mamba, kiboko, nyumbu,swalapala,nyani, ngedere,mbega,fisi pundamilia, palahala pamoja na aina za ndege wapatao 360,nyoka na wadudu.

Makosa ambayo yamefanyika kujenga barabara katikati ya hifadhi ya Taifa ya Mikumi yasirudiwe katika hifadhi nyingine ikiwemo hifadhi ya Taifa ya Serengeti kwa kuwa itaathiri mazingira, uhai wa wanyama na baionuai zilizopo katika hifadhi husika.

Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ina utajiri wa maliasili, uwanda mpana wa nyasi fupi,malisho mengi na maji ya kutosha pengine ndiyo maana hifadhi hiyo inapewa majina mengi kama vile Edeni ya Afrika kutokana na utajiri wa maliasili uliopo.

Hifadhi ya Taifa ya Serengeti yenye ukubwa wa kilometa za mraba 14,763 ilianzishwa mwaka 1951, ni Hifadhi ya Taifa ya pili kwa ukubwa nchini ikitanguliwa na hifadhi ya Taifa ya Ruaha yenye ukubwa wa kilometa za mraba 20,226.

Umaarufu wa hifadhi ya Taifa ya Serengeti kiuchumi unatokana na kuwa na misururu mirefu ya nyumbu wanaohama kwa makundi na kuvuka hata mpaka wa Tanzania hadi hifadhi ya wanyama pori ya Maasai Mara nchini Kenya.

Takwimu za TANAPA zinaonesha kuwa kila mwaka zaidi ya nyumbu milioni moja, pundamilia 200,000, swala tomi zaidi ya

300,000 na pofu 12,000 huunga misafara ya kutafuta malisho na maji katika hifadhi ya Serengeti.

Serikali ilitaka kujenga barabara ndani ya Hifadhi ya Serengeti ipite Mto wa Mbu-Engaruka-Loliondo- Kleins Gate-Serengeti-Mugumu-Nata na kuungana na ile ya Tarime-Musoma-Mwanza, hivyo kupunguza adha ya usafiri kwa wananchi wa maeneo hayo.

Miongoni mwa madhara ambayo yangeweza kujitokeza endapo barabara hiyo ingejengwa ndani ya Hifadhi ni uchafuzi wa maji kutokana na kumwagika kwa mafuta ya magari yanapoharibika, ongezeko la uwindaji haramu, ongezeko la vifo vya wanyama kwa kugongwa na magari na kupotea kwa uoto wa asili.

Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ni maarufu Afrika mashariki na duniani kote hali iliyosababisha shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu na Sayansi UNESCO kuitangaza Serengeti kuwa eneo la urithi wa Dunia kwa kuwa ndiyo eneo pekee duniani lililosalia kundi kubwa la wanyama wahamao.

Tatizo linaloikumba Hifadhi ya Taifa Mikumi la serikali kuruhusu barabara katikati ya hifadhi hiyo, linafanana na serikali ya Uganda mwaka 2006 kuruhusu mradi wa uchimbaji wa mafuta eneo la nchi kavu ziwa Albert ndani ya hifadhi ya Taifa ya Murchison.



Afisa Uhusiano wa Kampuni ya Uchimbaji Mafuta ya Tullow Oil Glorie Sebikali anakiri kampuni hiyo kukabiliwa na changamoto ya

uchimbaji wa visima vya mafuta,ujenzi wa mabomba na ujenzi wa barabara ndani ya hifadhi ya Taifa ya Murchson.

Mtaalamu wa Sera na Sheria za Madini nchini Uganda ambaye ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dundee nchini Uingereza Denis Kusaasiri anasema licha ya kwamba mafuta na madini yanaweza kuleta faida,ameshauri tathmini ya mazingira kufanyika kwa uangalifu mkubwa iwapo mradi unakuwa ndani ya hifadhi.

"Serikali inapoamua kuendesha mradi ndani ya hifadhi ni lazima kuzingatia sera na sheria mama za mazingira katika nchi husika na kufuata sheria za kimataifa za mazingira",anasisitiza mwanasheria huyo.

Fransis Mugerwa ni Mwandishi wa Habari nchini Uganda ambaye amefanya utafiti katika hifadhi ya Taifa ya Murchoson na kubaini vifo vya wanyama vya mara kwa mara vinavyotokea baada ya kugongwa na magari wakati wanavuka barabara na kwamba hata makazi ya asili ya wanyama na viumbehai yameanza kuharibiwa kutokana na shughuli za kibinadamu kwenye hifadhi hiyo.

Sekta ya utalii hapa nchini ni ya pili katika kuchangia pato la Taifa ambayo inachangia asilimia 17,hivyo ni lazima wanyamapori waliopo katika hifadhi za Taifa kulindwa na kuhifadhiwa.

**Albano Midelo ni Mchangiaji wa gazeti hili mawasiliano baruapepe:albano.midelo@gmail.com,simu 0784765917**